



Dkt. Devon Q. Horton, *Msimamizi*

SWAHILI

Bw. Dijon DaCosta, Sr., *Mwenyekiti wa Bodi*

Bi. Deirdre P. Pierce, *Mwenyekiti Msaidizi*

Bi. Anna Hill

Bi. Whitney McGinniss

Bi. Allyson Gevertz

Bi. Vickie B. Turner

Dkt. Joyce Morley

INAPASWA KUCHAPISHWA BILA KUKAWIA

4 Oktoba 2023

Mawasiliano:

Donald Porter, *Ed.D.*

678-481-4110

Carla Parker

404-734-1717

GaDOE Yasherehekea Shule Kadhaa za Mpango wa Title 1 za DCSD kwa Mafanikio na Maboresho Makubwa ya Kimasomo

(STONE MOUNTAIN, GA) – Mnamo tarehe 2 Oktoba, Idara ya Elimu ya Georgia (*GaDOE*) ilitoa orodha ya mwaka wa 2022-2023 ya *Shule Zinazotambulika* na *Zilizoboreka Zaidi (Distinguished and Reward Schools)*, ikiangazia shule nyingi kutoka Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb (*DCSD*). Tuzo ya *Shule Zinazotambulika* inatambua shule za mpango wa Title 1 zinazofanya vizuri zaidi katika Georgia, huku tuzo ya *Shule Zilizoboreka Zaidi* kitambua shule za mpango wa Title I zilizopata maboresho makubwa zaidi ya kimasomo.

Msimamizi Dkt. Devon Horton alisifu shule za DCSD zinazojitahidi na zinazofaulu kupata sifa hizi bora.

“Inatia moyo kuona kujitolea kwa ubora wa kimasomo na ukuaji wa wanafunzi ukikuzwa katika shule hizi bora za mpango wa Title 1,” Dkt. Horton alisema. “Kujitolea na bidii ya wanafunzi, walimu, wafanyakazi wetu na jamii nzima ya shule inaimarisha imani yetu kwamba kila mtoto anaweza kufaulu anapopewa usaidizi na fursa zinazofaa.”

Msimamizi wa Shule za Jimbo Richard Woods alikubaliana na maoni haya. Alisema, “Shule zilizojumuishwa kwenye orodha hizi zimefanya juhudi kubwa katika kukabiliana na vikwazo, changamoto, na kuleta mafanikio makubwa kwa wanafunzi wao. Ninawapongeza viongozi, walimu, wazazi na jamii za Shule Zinazotambulika na Zilizoboreka Zaidi za 2022-23 kwa kutoa fursa za kufaulu kwa wanafunzi.”

Shule Zinazotambulika ni miongoni mwa shule asilimia 5 zilizofanya vizuri zaidi za Mpango wa Title I Schoolwide na za Title I Targeted Assistance kulingana na alama za jumla za ustadi wa masomo ya hisabati na ELA kutoka kwa tathmini za jimbo nzima katika mwaka wa hivi majuzi zaidi. Shule za DCSD zilizotambuliwa ni pamoja na:

Shule ya Chesnut Elementary
DeKalb Early College Academy
Shule ya Laurel Ridge Elementary

Shule ya Livsey Elementary
Shule ya Robert Shaw Theme
Shule ya Wadsworth Magnet School for High Achievers

-ZAIDI-

Shule Zilizoboreka Zaidi ni miongoni mwa shule asilimia 5 zilizoboreka zaidi za Mpango wa Title I Schoolwide na za Title I Targeted Assistance ikilinganishwa na alama za ustadi wa masomo kutoka miaka miwili ya hivi majuzi ya tathmini za jimbo nzima. Shule za DCSD zilizotambuliwa kwa mafanikio haya ni pamoja na:

Shule ya Allgood Elementary
 Shule ya Avondale Elementary
 Shule ya DeKalb Agriculture Technology and Environment
 Shule ya DeKalb Elementary School of the Arts

Shule ya DeKalb PATH Academy Charter
 Shule ya Dunaire Elementary
 Shule ya Edward L. Bouie, Sr. Elementary
 Shule ya Hambrick Elementary

Shule ya Hawthorne Elementary
 Shule ya Idlewood Elementary
 Shule ya Kelley Lake Elementary
 Shule ya Laurel Ridge
 Elementary
 Shule ya Livsey Elementary
 Shule ya Robert Shaw Theme
 Shule ya Woodward Elementary
 Shule ya Wynbrooke Elementary

Bofya [HAPA](#) kwa vigezo vya kina vilivyotumika kwa utambuzi huu. Bofya viungo hivi kwa orodha kamili ya GaDOE ya [Shule Zinazotambulika](#) na [Shule Zilizoboreka Zaidi](#) kwa mwaka wa masomo wa 2022-2023.

XXX